**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI YA RAIS,**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA,**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA IRINGA.**

*Unapojibu tafadhali taja:*

Kumb.Na.IMC/C.40/23/366 12/06/2025

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Manispaa ya Iringa amepokea kibali cha Ajira mpya kutoka kwa Katibu Mkuu OR – Utumishi chenye **Kumb. Na. FA. 97/228/01/A/25** cha tarehe **29.04.2025.** Hivyo anapenda kuwatangazia watanzania wote wenye sifa kutuma maombi kwa nafasi Saba (07) kama zilivyoainishwa: -

### 1.0 MWANDISHI MWENDESHA OFISI DARAJA LA II (NAFASI 05)

### 1.1. KAZI NA MAJUKUMU

i. Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida na za siri;
ii. Kupokea wageni na kuwasaili shida zao na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa;
iii. Kutunza taarifa na kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba za kazi zingine;
iv. Kutafuta majalada na nyaraka zinazohitajika katika utekelezaji wa majukumu ya kazi;
v. Kupokea majalada na kusambaza kwa Maofisa walio katika Idara/Kitengo/Sehemu husika;
vi. Kukusanya, kutunza na kuyarejesha majalada na nyaraka sehemu zinazohusika.
vii. Kupanga dondoo na kufanya maandalizi ya vikao mbalimbali; na
viii. Kuandaa orodha ya mahitaji ya vifaa vya ofisi.

### 1.1.1 SIFA ZA MWOMBAJI.

Kuajiriwa Wahitimu wa kidato cha Nne au sita wenye Stashahada (Diploma) ya Uhazili au Cheti cha NTA level 6 ya uhazili. Aidha, wawe wamefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kiingereza maneno 100 kwa dakika moja na kupata programu za kompyuta za ofisi kama vile:- Word, Excel, PowerPoint, Internet, E-mail na Publisher kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

**1.1.2 NGAZI YA MSHAHARA.**
Kwa kuzingatia Ngazi za Mishahara ya Serikali - TGS C

**2.0 MSAIDIZI WA MAKTABA II (LIBRARY ASSISTANT) - NAFASI 1**
**2.1. KAZI NA MAJUKUMU**

i. Kuandikisha wasomaji;
ii. Kupanga vitabu katika rafu (Shelves);
iii. Kuazimisha na kupokea vitabu vinavyoazimwa;
iv. Kukarabati vitabu vilivyochakaa; na
v. Kazi nyingine atakazopangiwa na Mkuu wa Kituo.

**2.1.1 SIFA ZA MWOMBAJI**

Awe amehitimu Elimu ya Kidato cha Nne (IV). Awe amefaulu mafunzo ya Wasaidizi wa Maktaba (National Library Assistants Certificate Couse) yatolewayo na Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania au wenye cheti kinacholingana na hicho.

**2.1.2 NGAZI YA MSHAHARA.**
Kwa kuzingatia Ngazi za Mishahara ya Serikali - TGS B

**3.0 DEREVA WA MITAMBO DARAJA LA II - NAFASI 1**
**3.1 KAZI NA MAJUKUMU**

i. Kuendesha mitambo kikamilifu bila kusimamiwa;
ii. Kuweka vipimo mbalimbali vinavyotakiwa kufuatana na kazi anayofanya na jinsi anavyoelekezwa na kiongozi wa kazi hiyo;
iii. Kutoa huduma ya kwanza ya matengenezo ya mitambo na pia aweze kutoa maelekezo sahihi ya ubovu wa mitambo anapotakiwa kufanya hivyo;
iv. Kuandika vizuri 'log sheet' na kuweka kumbukumbu sahihi ya matumizi ya vifaa kwa mfano mafuta, grisi na vipuri;
v. Kuhakikisha kuwa mashine/mitambo inatumika kwa kazi zinazotakiwa;
vi. Kufanya usafi wa mtambo; na
vii. Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na Msimamizi wake.

**3.1.1 SIFA ZA MWOMBAJI.**
Awe na cheti cha Mtihani wa Kidato cha Nne (IV), mwenye leseni daraja 'G' ya uendeshaji mitambo pamoja na ujuzi wa kutunza vyombo mbalimbali vya mitambo hiyo, wenye uzoefu wa kuendesha mitambo kwa muda usiopungua saa mia tatu (300) au miezi mitatu (3) bila kusababisha ajali pamoja na vyeti vya mafunzo vilivyowapatia sifa ya kupata daraja husika

**3.1.2 MSHAHARA**
Mshahara atalipwa kwa kuzingatia viwango vya Serikali -TGOS A

**MASHARTI YA JUMLA**

i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania wenye umri wa miaka 18 na usiozidi miaka 45 .

**ii. Waombaji wenye ulemavu wanahamasishwa kutuma maombi na wanapaswa kuainisha kwenye mfumo wa kuombea ajira Ulemavu walionao kwa ajili ya taarifa kwa Sekretarieti ya ajira katika Utumishi wa Umma.**

iii. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anuani inayotumika, namba za simu zinazopatikana na anuani ya barua pepe (E-mail Address) pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.

**iv.** Maombi yote yaambatane na vyeti vya Elimu na taaluma vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya Kidato cha Nne au Kidato cha Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika **Postgraduate/Degree/Advanced Diploma/Diploma/Certificate – Cheti cha Mtihani wa Kidato cha nne na cha Sita, Computer Certificate, - Vyeti vya Kitaaluma (Proffessional Certificate from Respective Boards).**

v. Wasailiwa watakaowasilisha **Testimonials, Provisional Results, Statement of results, hatiza matokeo za kidato cha IV na VI (form V and form VI results slips) HAVITAKUBALIWA NA HAWATARUHUSIWA KUENDELEA NA USAILI**.

**vi.** Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na Vimethibitishwa na Mamlaka husika **(TCU, NECTA na NACTVET).**

vii. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.

viii. Waombaji kazi wa kada ya Dereva wa Mitambo II wenye leseni Daraja G wanapaswa KUAMBATISHA vyeti vya mafunzo ya Udereva vilivyowapatia sifa ya kupata daraja husika.

ix. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika **Waraka Na. CAC. 45/257/01/D/140** wa tarehe **30 Novemba, 2010**.

x. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.

xi. Waombaji watakaowasilisha taarifa na sifa za kughushi watachukuliwa hatua za kisheria.

xii. Wasailiwa ambao majina yao yanatofautiana katika nyaraka zao wanapaswa kuwasilisha Hati ya Kiapo cha Kubadili Jina (Deed Poll) iliyosajiliwa na Wizara ya Ardhi.

**xiii.** Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **25 Juni, 2025.**

**MUHIMU:** Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya Elimu, anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa:

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Manispaa ya
Iringa,
S.L.P 162,
**IRINGA.**

xiv. Maombi yote ya kazi yatumwe kwenye mfumo wa kielekroniki wa ajira (Recruitment Portal) kupitia anuani ifuatayo https://portal.ajira.go.tz/ (Anuani hii pia inapatikana kwenye Tovuti ya Sekretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa ‘Recruitment Portal’).

xv. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulio ainishwa katika tangazo hili **HAYATAFIKIRIWA.**

Tangazo hili limetolewa na;

**MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA IRINGA.**